JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS (TAMISEMI)
MKOA WA DODOMA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA

Fax:
Simu: 0625 299 341 / 0784 326 541/
Email: mseniomary@yahoo.com

Shule ya Sekondari Msakwalo,
S. L. P. 830
CHEMBA
0622 754 006

Kumb. Na. MSKLSS/ADMN/FV 2018/201 15/05/2018

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi……

S. L. P ……

Ndg:

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MSAKWALO MWAKA 2018.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2018/2019** tahasusi (combination) ya ……..
2. **(a)** Shule ya Sekondari **MSAKWALO** ipo umbali wa **Kilometa 164**, Kaskazini mwa manispaa ya **Dodoma**, ukifika Dodoma stendi Kuu (stendi ya Mikoani) uliza **stendi ya Jamatini**, hapo utapata daladala za kukupeleka stendi ya **Chang'ombe Juu** ukifika huko, uliza mabasi ya **NIA NJEMA au FALCON (stendi ya mabasi ya Usandawe)**, nauli ni **Tsh 8000/=** kwa mtu mmoja hadi unafika Msakwalo Sekondari kwa watakao tokea Dodoma, ukiingia katika basi mwambie Kondakta akushushe **Msakwalo Sekondari kibaoni, Pia nauli ni Tsh 5000/= kwa watakao tokea Singida. J**engo la utawala lipo umbali wa mita 200 kutoka Kibao cha shule.

   Ratiba ya magari

   - Kwa Singida OVADA (Msakwalo) magari yapo kila siku.
   - Kwa Dodoma- OVADA (Msakwalo) gari lipo **Jumanne** (NIA NJEMA BUS) linaondoka Dodoma Saa moja kamili asubuhi. **Jumatano** (FALCON BUS) linaondoka Dodoma saa moja kamili asubuhi. **Jumamos**i (FALCON BUS) linaondoka Dodoma saa moja kamili asubuhi(01:00 asbh) . **Jumapili** (NIANJEMA BUS) linaondoka Dodoma Saa moja kamili asubuhi.

     Hivyo unashauriwa kufika Dodoma siku moja kabla ya safari na ukate tiketi mapema.

   (b) Wale wanaotoka kanda ya kaskazini, kanda ya ziwa na Mkoa wa Kigoma washuke Mkoani Singida waulizie magari ya kuelekea USANDAWE au Msakwalo (OVADA). Sekondari iliyopo Kijiji cha OVADA ,Wilayani Chemba Mkoani Dodoma kwa maana shule yetu ipo mpakani mwa mkoa wa Singida.

   Penye utata wowote piga namba hizo hapo juu, **karibu sana Msakwalo Sekondari.**

   Muhula wa masomo unaanza tarehe 02/7/2018. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 02/7/2018. Mwisho wa kuripoti ni wiki mbili baada ya kufungua shule.

3. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

   2.1 Sare za shule.

a) Sare ya shule hii ni

- Suruali mbili rangi ya dark blue wakati wa masomo, zisiyo bana (siyo model)
- Suruali mbili nyeusi isiyo bana (isiyo model) baada ya masomo. (shamba dress).
- T-shirt 2 rangi nyekundu zisizo na maandishi (shamba dress)
- Truck suit 2 rangi nyekundu zenye michirizi myeupe za kupwaya.
- Shati mbili nyeupe mikono mirefu
- Sweta 1 rangi ya dark blue.
- Tai ya dark blue, ni sehemu ya uniform ukiwa darasani.
- Viatu vyeusi jozi 2 vya kufunga na kamba, visigino vifupi wakati wa masomo.
- Socks nyeupe jozi 2 wakati wa masomo na jozi 2 za kijivu wakati wa michezo.
- Viatu aina ya raba jozi 1 kwa ajili ya michezo.
- Kandambili za kuogea, (zitumike bwenini tu).

3.2 **Ada na michango ya shule.**

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi elfu sabini (Tsh 70,000.00/=) kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa elfu thelathini na tano (Tsh 35,000/=) kwa Mwanafunzi wa bweni kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule nambari A/C- 5021200102 (NMB) **MSAKWALO SECONDARY SCHOOL,** katika Benki ya **NMB** tafadhali **andika jina la Mwanafunzi na sio Jina la mzazi kwenye pay in slip ambayo ataiwasilisha shuleni.**

b) Michango inatakiwa kulipwa na kila Mzazi ni:-

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma.
iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine hapa shuleni.
v. Aje na bima ya afya NHIF au CHF, gharama zingine za matibabu ni wajibu wa mzazi au mlezi.
vi. Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima ya ndani.
vii. Shilingi 20,000/= mchango **wa ku pampu maji kwa mwaka**.
viii. Fedha ya tahadahari Tsh 5,000/= fedha hiyo hairudishwi.
ix. Michango yamahafali kidato cha nne na kidato cha sita mtajulishwa.

Jumla ya michango ni Tsh 116,000/=

Jumla ya ada na michango mingine kwa mwaka ni Tsh. 186,000/=

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni ni:-

i) Ream ya karatasi nyeupe isiyo na mistari bunda mbili (02)
ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi (kulingana na mchepuo wake)
iii) Scientific calculator.
iv) Godoro lenye foronya. Urefu futi6, upana futi $2\frac{1}{2}$ (ft mbili na nusu) unene wa inchi nne (4).
v) Mashuka pair 2 rangi ya pink au blue. Blanket 1(Kuna baridi kali), chandarua 1 rangi ya blue.

vi) Vyombo vya chakula (sahani ya mfupa, bakuli ya mfupa, kijiko na kikombe).
vii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
viii) Reki 1 kwa HGK, jembe 1 kwa HGL na kwanja 1 kwa wote.
ix) Ufagio wa ndani 1 (special bloom1) na ufagio wa nje wa cherewa 1

4. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa/ utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana na mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu, muda wote kwa wenye ndevu kata ndevu zako.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa.
xi. Kusabaisha mimba kwa wanafunzi au nje ya shule (kwenye jamii inayozunguka shule yetu).
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
NB. Huruhusiwi kuja na simu shuleni, hatuna utaratibu wa kupokea na kuhifadhi simu za wanafunzi.
Mwanafunzi atatumia simu ya shule tu ambayo anakuwa nayo Patroni kufanya mawasiliano na mzazi au mlezi kwa siku za jumamosi na jumapili tu.
Pia mzazi/ mlezi awasiliane na mwanafunzi kupitia simu ya shule tu.
xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xviii. Kwenda nyumbani kwa walimu bila sababu maalum.
xix. Kuja na nguo zilizo nje ya maelekezo ya sare za shule, nguo za nyumbani mwanafunzi hatakiwi kuwa nazo.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

TUNAKUTAKIA SAFARI NJEMA KUFIKA MSAKWALO SEKONDARI.

Jina la Mkuu wa Shule <u>MSENI A OMARY.</u>

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

CHEMBA DISTRICT COUNCIL

FARKWA HIGH SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

(**To be completed by Medical Officer in respect of all Form V entrants**)

Pupil's full name: _____

Age: _____ Years. Sex: _____

Blood count (Red and White) _____

Stool Examination _____

Syphilis and other venereal diseases test _____

T. B Test _____

Eye Test _____

Ears Test _____

Spleen _____

Abdomen _____

Urine for plamotest _____

Test for pregnancy (For girls only) _____

ADDITIONAL INFORMATION

(If any) e. g physical defects impartment,

Infections, chronic or family diseases etc _____

_____

_____

I certify that the above pupil is fit to pursue studies at Msakwalo Secondary School.

Station _____ Signature _____

Date _____ Designation _____

NB: This form should be completed and submit to school on arrival